

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA TUNDURU

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya)

MKOA WA RUVUMA



OFISI YA MKURUGENZI
S.L.P 275
TUNDURU

SIMU NA. 2680004

FAX No. 2680208

Barua pepe: info@tundurudc.go.tz

29/05/2017

TAARIFA KWA UMMA

HALMASHAURI KUPITIA IDARA YA MAENDELEO YA JAMII INARAJIA KULIPA JUMLA YA SHILINGI MILIONI 440,757,509.00 RUZUKU YA WALENGWA WA KAYA MASKINI.

Mpango wa kunusuru kaya maskini wilayani Tunduru unatekelezwa katika Vijiji 88 kati ya Vijiji 157 vya Halmashauri ambayo ina wanufaika wapatao 13,916 kaya ambazo zinapata ruzuku ya mwezi na huduma za Elimu, na Afya.

Halmashauri ya wilaya ya Tunduru kupitia Idara ya Maendeleo ya jamii kitengo cha Tasaf wanaendelea na zoezi la ugawaji wa fedha za ruzuku kwa wanufaika katika vijiji vyote zoezi hili linaanza baada ya kufungua dirisha la malipo hufunguliwa kuanzia tarehe 22/mei na kufungwa tarehe 03 june.

Aidha Kaimu Mratibu wa TASAF wilaya **Ndg Muhidin Shaibu** amesema dirisha la malipo limefunguliwa tayari kwa taratibu za malipo ya walengwa na wanatarajia kufanya zoezi hilo kwa muda wa siku nne na wanatarajia kulipa jumla ya shilingi milioni 440,757,509.00 kwa mwezi mei na june 2017.

Aidha wakufunzi na wasimamizi wote watatoa mafunzo kwa wanufaika kabla ya kuanza na zoezi la kugawa fedha kwa walengwa, ikiwa ni pamoja na kuhamasisha walengwa kujiunga na mfuko wa afya ya jamii (CHF) na kuwahimiza wazazi kuwasimamia wanafunzi kuhudhuria shule, kusikiliza kero za wanauifaka wanazokumbana nazo walengwa wa tasaf.

Aidha wanufaika watafundishwa njia za kuibua miradi ikiwa ni pamoja na kushiriki katika vikundi vya kuweka akiba na kukopa ili kuweza kuwekeza katika miradi ya maendeleo na kujikwamua kiuchumi na kuondokana na umaskini.

Imetolewa na
Theresia Mallya
Afisa habari (W)

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA TUNDURU

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya)

MKOA WA RUVUMA



OFISI YA MKURUGENZI
S.L.P 275
TUNDURU

SIMU NA. 2680004

FAX No. 2680208

Barua pepe: info@tundurudc.go.tz

29/05/2017

TAARIFA YA MALIPO YA UHAWILISHAJI FEDHA KWA WALENGWA CCT KWA KIPINDI CHA MIEZI MEI - JUNI 2017

Halmashauri ya wilaya ya Tunduru imepokea jumla ya tsh 440,757,509.00 kwa ajili ya malipo ya walengwa kwa kipindi cha mwezi mei na juni 2017 pamoja na fedha za usimamizi ngazi ya wilaya, kata na vijiji. Na katika mapokeo hayo jumla ya kata 13,916 zilitarajiwa kulipwa kutika katika vijiji 88 vinavyotekeleza mradi wa kunusuru kaya maskini.

Aidha akitoa taarifa ya malipo hayo kaimu mratibu wa TASAF wilaya ya Tunduru kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji W Ndg Muhidin Shaibu alisema kuwa malipo yalifanyika kuanza tarehe 29/05/2017 hadi tarehe 05/06/2017 katika vijiji vyote 88 vya mradi na jumla ya kaya 13,905 zimelipwa sawa na asilimia 99.9 na kaya 11 ndio hazikulipwa kutoka na walengwa kufariki, ujumbe wa Halmashauri ya kijiji na kuhama makazi ambapo jumla ya tsh 248,000.00 kilirejeshwa TASAF makao makuu.

Changamoto kubwa ambayo imejitokeza katika malipo ya awamu hii ni baadhi ya serikali za vijiji kushindwa kuweka benki fedha za mchango wa tasaf kwa kijiji kutokana na Akaunti za vijiji kulala (dormant), kukosekana kwa huduma CHF kwa vijiji vinavyohudumiwa na Hospitali za taasisi za dini (mission) na watendaji wa vijiji kushindwa kuwasilisha taarifa za marekebisho ya walengwa katika ofisi za mratibu wa tasaf wilaya, ikiwa ni taarifa za Kliniki, Shule za Msingi na waliofaulu na kuendelea na Elimu ya Sekondari.

Kaimu Mratibu TASAF wilaya alisema kuwa halmashauri iweka mipango mikakati ya kukabiliana na changamoto hizi ikiwa ni pamoja kuagiza vijiji ambavyo akaunti zimelala kwenda kuzipa uhai mara moja, mganga mkuu wilaya kufanya mawasiliano na uongozi wa hospitali za taasisi za dini (mission Hospital) ili kuona kama kuna uwezekano wa wananchi kupata huduma za CHF, kufanya ufuatiliaji kwa watendaji wa vijiji ili waweze

kuwasilisha marekebicho ya taarifa za walengwa kwa wakati ili zifanyiwe kazi kwenye mfumo.

Hitimisho

Hata hivyo alisema walengwa wa TASAF wamefanikiwa kwa kiasi kikubwa sana katika kubadilisha hali za maisha yao, kwa kuweza kusomesha watoto, kupata mlo kamili, kuanzisha miradi ya ufugaji wa kuku na mbuzi, kuboresha makazi yao na kufufua mashamba ya korosho kwa kutumia ruzuku wanayopokea kupitia mradi wa kunusuru kaya maskini.

Imetolewa na
Theresia Mallya
Afisa habari (W)